
# KUSHIRIKI KWA WANANCHI KATIKA MCHAKATO WA BAJETI KATIKA KAUNTI ZAO



## Mchakato wa Bajeti katika Kaunti

### Je, Ugatuzi ni nini?

Ugatuzi ni kubadili namna uamuzi unavyofanywa na utoaji wa huduma nchini Kenya. Fikiria huduma unazozijali kama vile, afya, maji, masomo au makao. Ni nani anaye amua na kutahmini huduma itakayopewa kipaumbele kifedha? Katika mfumo mpya wa ugatuzi kuna sehemu mbili za utawala; ile ya Kaunti na ile ya Kitaifa. Kaunti zina majukumu ya baadhi za huduma. Serikali ya kitaifa vile vile. Lakini serikali zote mbili zinafaa kufanya kazi kwa pamoja zikishirikiana. Kaunti zina majukumu juu ya elimu ya kimsingi ya utotoni (kama vile ya chekechea), soko, vituo vya afya vya Kaunti, makao, maji, usafi, na zinginezo. Kaunti zinastahili kutunga fedha kwa ajili ya huduma hizi kila mwaka. LAZIMA wananchi wahusishwe katika michakato ya bajeti.

### Mwananchi atashiriki vipi katika mchakato bajeti katika mfumo wa ugatuzi?

Kama mwananchi, umepewa mamlaka katika mfumo wa ugatuzi. Mamlaka haya pia yana majukumu. Unastahili kushiriki katika maamuzi yanayohusu maisha yako kama vile kuchangia katika kubuniwa kwa bajeti na mipangilio ya serikali. Jukumu lako ni kuelewa kinachofanywa na serikali na kuhakikisha kuwa umehusika kikamilifu katika maamuzi inavyowezekana.

Je, ni jambo lipi ambalo umefanya katika mchakato wa kuunda bajeti? .......

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

## Bajeti ni nini?

Huu ni mukhtasari wa fedha serikali inazokusudia kupata na kutumia kwa muda fulani. Bajeti husaidia serikali kuamua sehemu zitakazopewa kipaumbele na kuzitengea fedha za kutosha. Huu ni mpangilio wa matumizi ya fedha wa mwaka kulingana na mipangilio ya maendeleo ya Kaunti husika. Kwa jumla, mchakato wa bajeti katika serikali za Kaunti na ya Kitaifa ni mmoja. Mchakato wa bajeti hufanywa kila mwaka na huchukua **hatua nne.**

1. Mwanzo, serikali ya utendaji (ile ya fedha katika Kaunti) inapendekeza mpango wa matumizi ya fedha

2. Pili, mapendekezo haya yanajadiliwa na kupitishwa na Bunge la Kaunti. Huu pia ndio wakati ambapo Kamati ya Bajeti ya Kaunti hufanya vikao vya faragha kujadili bajeti. Wewe kama mwanchi unahusika kwa wakati huu. Tarehe na mwezi wa vikao hivi zitajadiliwa hapa chini katika mzunguko wa bajeti.

3. Tatu, bajeti inatekelezwa na serikali ya utendaji ya Kaunti

4. Mwisho, kuna hatua ya kupitia ili kuhakikisha kuwa bajeti imetekelezwa inavyostahili. Haya hufanywa na Bunge la Kaunti, Mkuu wa Bajeti na Mkaguzi Mkuu.

## Ni Tarehe zipi za kuangaziwa katika mchakato wa bajeti katika Kaunti?

Kwa kawaida, hii huitwa mzunguko wa bajeti katika Kaunti. Hapa, wananchi hushirikishwa kulingana na kipengee cha 201 cha Katiba ya Kenya. Kipengee hiki kimetoa kanuni zinazohusu fedha za umma ikiwemo uwazi na uwajibikaji katika maswala ya fedha za umma. Kushirikishwa kwa wananchi

katika bajeti na katika hatua za kutoa maamuzi kumezingatiwa mno. Pia, hili limezingatiwa na Sheria ya Bunge ya Usimamizi wa Fedha za Umma na ile ya Serikali za Kaunti katika upande wa nne.

## Wananchi wanaombwa kutilia tarehe hizi maanani kuhakikisha kuwa fursa yao ya kushiriki imetumika vizuri

| Wakati | Shuguli |
|---|---|
| **Agosti 30** | Afisi ya fedha (hazina) katika Kaunti inatoa ujumbe kwa idara zote kuzifahamisha kuwa hatua za kutunga bajeti zitaanza. Hili linakusudia idara hizo zitoe maombi ya fedha kwa serikali ya Kaunti.<br><br>Ujumbe huu ni wa maana kwa kuwa unatoa, kwa kina, mpangilio jinsi wananchi watashiriki kabla ya bajeti kuwekwa mikononi mwa Kaunti. Wanachi wanaweza kupata ujumbe huu kupitia kwa ofisi za wawakilishi wa wodi zao. |
| **Septemba 1** | **Kaunti zinatayarisha na kutoa mpangilio wa Maendeleo katika Kaunti kwa bunge la Kaunti ili upitishwe. Inalazimu uma ufahamishwe kuhusu mpangilio huu kabla ya siku saba** |
| **Septemba 1 hadi Februari 15** | Wakati huu, idara za serikali ya Kaunti hujadiliana na umma na washikadau wengine. Maoni ya umma uhusishwa katika utunzi wa mapitio ya bajeti za Kaunti na Karatasi la mtazamo (CBROP) |
| **Januari 1** | Kufikia Januari ya kila mwaka, Tume inayohusika na kugawa kwa mapato inastahili kutoa mapendekezo bungeni kuhusu kugawa kwa mapato baina ya serikali kuu na za kaunti |
| **Februari 15** | Miswada ya mgawanyiko wa mapato na ule wa mgao wa mapato kwa kaunti inapelekwa bungeni |

| | |
|---|---|
| **Februari 28** | Tarehe ya mwisho ya kuwakilisha Karatasi la mikakati ya fedha katika bunge la kaunti |
| **Machi 16** | Tarehe ya mwisho yabunge  kupitisha miswada ya mgawanyiko wa mapato na ule wa mgao wa mapato katika kaunti |
| **Aprili 30** | Serikali tekelezi ya kaunti (Gavana na kamati tekelezi ya kaunti) hutayarisha na kutoa makadirio (mpangilio wa matumizi unaokusudiwa) kwa bunge la kaunti ili yajadiliwe, yarekebishwe na kupitishwa. Bunge la kaunti linaweza kujadili na kubadilisha bajeti wakati wowote kati ya Aprili 30 na Juni 30. |
| **Mei** | Wakati huu, kamati ya bajeti ya kaunti inatarajiwa kufanya vikao vyo faraga kuhusu bajeti |
| **Juni** | Mswada wa fedha za kaunti unapelekwa katika bunge la kaunti |
| **Juni 30** | Huu ndio mwisho wa mwaka wa fedha na tarehe ya mwisho kwa bunge za kaunti kuamuru matumizi ya fedha kwa mwaka mpya wa bajeti. |
| **Oktoba 30** | Serikali ya Kaunti huchapisha ripoti ya utekelezaji kati ya Julai na Septemba. Serikali ya Kitaifa inastahili kufanya hili kufikia Novemba 15 kila mwaka. |

Ukitazama ratiba hii ya bajeti, je, ni miezi ipi ambayo utakuwa na fursa ya kushiriki katika mchakato wa kuunda bajeti?................................................

Utakuwa na lipi la muhimu utakalo ongezea katika warsha hizi?.................

..........................................................................................................................

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Machi 1** | Bunge linazingatia ripoti kuhusu Habari ya Sera za Bajeti na kupitisha maazimio (baada ya kufanyiwa marekebisho au bila ya marekebisho) | **Kamati ya Bunge la Kitaifa kuangazia Mswada wa Mgao wa Mapato** | Bunge la Kaunti kuangazia Mikakati ya Fedha ya Kaunti na Kuipitsha ikiwa na au bila ya marekebisho |
| **Machi 15** | | | |
| **Aprili 30** | Kuwasilishwa kwa makadirio ya kina ya bajeti ya serikali kuu bungeni ikiwemo Mgao kutoka kwa Hazina ya Usawa | Kamati ya Bunge la Seneti kuangazia Mswada wa Mgao wa Mapato na kutoa ripoti kwa Bunge | Makadirio ya Bajeti ya kina kuwasilishwa kwa Bunge la Kaunti |
| | Kuwasilishwa bungeni kwa makadirio ya kina ya bajeti ya Mahakama na Bunge | | |
| **Mei 15** | Waziri wa fedha kuwasilisha maoni kuhusu makadirio ya bajeti ya Mahakama na Bunge | | Kamati ya Bunge kuangazia makadirio na kutoa ripoti kwa Bunge |
| | Kamati ya Bunge la Kitaifa kuangazia makadirio na ripoti | | |
| **Mei 30** | Makadirio kupitishwa na Bunge (kabla ya sheria ya matumizi ya fedha ya tarehe 30 Juni) | Bunge kuangazia Miswada ya Mgao wa Mapato kwa mara ya pili (ikiwa au bila ya marekebisho) | Kupitishwa kwa makadirio na Bunge la Kaunti (kabla ya Sheria ya Matumizi ya Fedha ya tarehe 30 Juni) |
| **Juni 30** | Mswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha kupitishwa na Kutiwa sahihi na Rais | | Sheria ya Matumizi ya Fedha ya Kaunti sharti iwe imepitishwa |

## Baadhi ya Maswali Mkaaji wa Kaunti ya Jiji la Nairobi anaweza kuuliza katika vikao vya hadhara vya mchakato wa utunzi wa bajeti

Serikali za Kaunti zinapowasilisha bajeti zao, kuna umuhimu kwa wananchi kuuliza maswali Fulani – kuhakikisha kuwa bajeti zinazingatia mambo wanayopatia kipaumbele. Haya ni maswali **MANNE** (baadhi ya maswali) ambayo mwananchi anaweza kuuliza kuhusu bajeti inapowasilishwa Mwezi Aprili.

### 1. Je, ni sababu zipi zilizotolewa na viongozi Wangu kuhusu maamuzi waliyoyatoa wakitunga bajeti?

Swali hili linauliza ikiwa kuna masimulizi katika bajeti yanayoelezea sababu za maamuzi fulani yaliyofanywa na Kaunti. Kila bajeti lazima iwe na maamuzi kuhusu matumizi ya kiwango fulani cha fedha ikizingatiwa kuwa hazitoshi kutimiza yote. Kuna namna nzuri za kugawa fedha, lakini ni vyema kutoa maelezo kuhusu vipaumbele na sababu za kufanya maamuzi fulani. Si vyema kutoa ujumbe kuhusu bajeti bila kutoa maelezo.



## 2. Ni sehemu zipi zilizopewa kipaumbele katika bajeti yangu?

Tunapozungumzia sehemu zinazopewa kipaumbele, kwa jumla tunamaanisha sekta zilizopewa mgao wa juu zaidi. Hii ni njia mojawapo ya kuelewa maamuzi yaliyotolewa na vipaumbele. Unaweza kutambua sehemu iliyopewa kipaumbele kwa kulinganisha bajeti ya sasa na ile ya mwaka uliopita au ukilinganisha na bajeti za kaunti zingine sawia.

## 3. Je, Bajeti yangu inaelezea mahali ambapo (wodi au eneo bunge) miradi ya Maendeleo itafanywa?

Ili kufahamu fika jinsi bajeti inagawa rasilmali kwa usawa, tunataka kujua mahali Nyumba na mijengo itakapokuwa. Hili linaitaji ujumbe kuhusu matumizi usambazwe zaidi ya kaunti (hadi kwa kaunti ndogo na hata wodi). Kwa jumla, ujumbe huu unafaa kuwa katika sehemu ya bajeti inayozungumzia matumizi ya Maendeleo.

## 4. Je, ni fedha ngapi Kaunti yangu inakusudia kukusanya kutoka kwa ushuru inayotoza na je, hilo linawezekana?

Kaunti hupata fedha kutoka kwa serikali kuu na pia kutoka kwa ushuru zinazotoza. Kaunti nyingi zimekadiria, kwa viwango vya juu, mapato kutokana na rasilimali zao. Ili kujua kuwa itawezekana au la, mtu anaweza kulinganisha makadirio haya na jinsi mamlaka ya miji na vijiji yalivyokuwa yakipata mapato kutoka kwa rasilimali hizo. Ujumbe huu unaweza kupatikana katika ripoti ya mashirika yanayofaidi umma (PBO) ya 2012/2013.

Ni sehemu zipi ulizozipa kipaumbele katika wodi yako kwa bajeti inayopendekezwa sasa?.................................................................................

.......................................................................................................................

## Je, viongozi wa kisiasa wa Serikali kuu na za Kaunti wana majukumu yepi katika mchakato wa kuunda bajeti za Kaunti?

### Wabunge wa Bunge la Kitaifa

Wabunge wa Bunge la Kitaifa wanao jukumu la kutathmini jumla ya fedha zilizopo kwa ajili ya matumizi ya kaunti. Lakini hawana jukumu la kuamua zitakavyotumika. Baada ya Rais na mawaziri kuanza utekelezaji wa mipangilio ya kitaifa na bajeti, wabunge hawa lazima wafuatilie utekelezaji huo na hata kuchunguza matumizi yeyoyte mabaya ya fedha za umma.

### Maseneta (Seneti)

Bunge la Seneti linawakilisha kaunti na lina jukumu la kutetea uhitaji wa kaunti katika bunge lao. Mbali na kuwa wabunge wa bunge la Taifa, wanaochaguliwa kuwakilisha maeneo bunge, maseneta huchaguliwa kutoka kwa kaunti. Jukumu la seneti katika kuunda bajeti ni kutathmini jumla ya fedha kaunti zinazopata kila mwaka. Seneti pia inahitajika ifuatilie mgao wa ushuru wa kitaifa kwa serikali za kaunti.

### Gavana

Gavana hupendekeza mipango na bajeti kila mwaka ili ziongoze ukuaji wa Maendeleo katika kaunti. Mara mipango hiyo na bajeti zinapopitishwa (huenda zikapitishwa baada ya marekebisho), Gavana na wanachama wa kamati tekelezi za kaunti huchukua jukumu la kutekeleza mipango na bajeti hizo.

### Wabunge wa Bunge za Kaunti (MCAs)

Wabunge wa bunge za kaunti, kama vile wale wa bunge la kitaifa, wana jukumu la kujadili mipango na bajeti za kamati tekelezi (gavana na mawaziri

wa kaunti), kuzirekebisha na kuzipitisha. Mara Gavana na mawaziri wanapoanza kutekeleza mipango na bajeti, bunge la kaunti lazima lifuatilie utekelezaji huo na hata kuchunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

Je, kwa fikira zako, majukumu au kazi za wasimamizi wa wodi katika eneo lako ni zipi?..........................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

## Wawakilshi wa Akina Mama Katika Kaunti

Wawakilishi wa akina mama katika kaunti wanafaa kuangazia maswala ya jinsia katika kaunti. Pia, wanafaa kuhakikisha kuwa wamehusishwa katika bajeti.



## Mbinu zilizopo za kuwawezesha wananchi kushiriki katika mchakato wa kuunda bajeti katika kaunti zao

Kushiriki kwa wananchi katika mfumo wa ugatuzi ni wa muhimu mno. Hili ni kulingana na sheria. Kuna aina nyingi ambazo wananchi wanaweza kushiriki katika undaji bajeti. Mbinu zingine ni rasmi ilihali zingine zinahitaji ubunifu wa wanachi. Inamlazimu Gavana ahakikishe kuwa wananchi wameshiriki katika sera za maendeleo, mipangilio na utoaji wa huduma katika kaunti. Zifuatazo ni kanuni mbalimbali ambazo wananchi wanaweza kutumia ili wahusike katika mchakato wa kuunda na kutekeleza bajeti.

### 1. Bajeti ya Kaunti na Warsha za Kiuchumi

Sheria ya bunge kuhusu Usimamizi wa Fedha za Umma imebuni kuundwa kwa Warsha ya Bajeti na Uchumi ya Kaunti ambayo inaongozwa na Gavana. Warsha hii inawapa wananchi nafasi ya kutoa maoni yao, kuongezea na hata kupendekeza katika mipangilio, vipaumbele na kuundwa kwa bajeti. Hawa ni lazima wahusishwe katika warsha hii; kamati tekelezi ya kaunti, wawakilishi wa vikundi vya kitaaluma, mashirika yasiyo ya serikali, wanawake, walio na ulemavu, mashirika ya kidini na wengineo. Maoni ya wananchi huunganishwa katika stakabadhi kama vile ile karatasi ya mikakati ya kifedha.

### 2. Maombi

Wananchi wanaweza, kupitia kwa bajeti na vipaumbele vilivyopendekezwa, kutayarisha maombi yaliyotiwa sahihi wakitoa maoni tofauti yanayopendekeza vipaumbele na mgao wa fedha.

### 3. Warsha za Wananchi

Warsha hizi huandaliwa na kaunti katika ngazi zote za utawala wa kaunti, kaunti ndogo, wodi na vijiji. Hili linahakikisha kuwa wananchi wote

wamepata fursa sawa ya kushiriki bila kubaguliwa. Hata hivyo, ni wajibu wa kila mwananchi kuelekea katika afisi husika za kaunti na wodi kudai na kushiriki katika mikutano hii kwa lengo la kutoa mchango wao kisahihi.




## 4. Jukwaa na Mikakati ya Mawasiliano katika Kaunti

Kipengee cha 35 1 (a) na (b) cha Katiba ya Kenya kinalazimu serikali za kaunti zichapishe na zitangaze habari zinazohusu wananchi – moja kwa moja – ikiwemo habari inayohusu bajeti. Wananchi wana haki ya kupata habari muhimu inayoathiri maisha yao ya kila siku.

## 5. Mikutano ya Kamati ya Bajeti ya Kaunti

Kamati ya Bajeti na Mgao wa Matumizi ya bunge la kaunti ina jukumu la

kikatiba la kuandaa mikutano ya hadhara ampambo wananchi wanaweza kuzungumzia vipaumbele vyao. Wananchi wamepewa fursa ya kushawishi matokeao ya bajeti kabla ipitishwe.

## 6. Maoni

Wananchi pia wanaweza kutayarisha, kwa pamoja, maoni na kutumia wawakilishi wao wa wodi kuyawasilisha kwa kamati husika ya kaunti ili yaangaziwe. Maoni haya lazima yaangazie umaalum wa usawa wa wapiga kura katika bajeti yote.


## 7. Karatasi la Kupitia na Kutazama Bajeti ya Kaunti

Hili ni karatasi ambalo huangalia hutendaji wa serikali kuhusu bajeti kila mwisho wa mwaka wa bajeti. Karatasi hili linafaa liwe la muhimu kwa wananchi. Linaelezea tofauti zozote zilizopo kati ya bajeti ya mwaka wa bajeti uliopita na utekelezaji halisi wa bajeti au tofauti zilizotokea ilipokuwa ikitekelezwa. Wananchi wanafaa wawe na nakala ya karatasi hili kama namna ya kufuatilia bajeti ili waiunge au waelezee tofauti zilizoshuhudiwa mashinani na kuzijumuisha katika ripoti ya wananchi ya mwaka wa bajeti. Wananchi watalipata wapi?

## Bajeti ya Kaunti ya Jiji la Nairobi: Uchambuzi wa Jumla wa Bajeti ya Mwaka 2014/2015 (Kwa ufahamu wako)

i. **Je, jumla ya bajeti ya Kaunti yangu ni ipi?**

Jumla ya bajeti ya Kaunti ya Jiji la Nairobi ni shilingi bilioni 25.2. Asilimia 59 (bilioni 14.9) ni ya matumizi ya kawaida/kulipa mishahara, asilimia 30 (bilioni 7.5) ni ya maendeleo, asilimia 11 (bilioni 2.7) ni ya kulipa madeni. Haya yamefafanuliwa katika picha ya pili ifuatayo





Picha ya 2**: Jumla ya Matumizi ya mwaka wa 2013/14**

ii. **Fedha hizi zinatoka wapi?**

**Mapato ya Kaunti ya Jiji la Nairobi Bilioni 15.1**

**Mgao Kutoka kwa Serikali Kuu Bilioni 9.5**

**Misaada ya Kutegemea kutoka kwa Serikali Kuu Milioni 743.17**




Picha ya 3: **Fedha kwa Kaunti**

Kutokana na **Picha ya 3** iliyopo hapa juu**,** bajeti ya mwaka wa 2013/14 ya Kaunti ya Jiji la Nairobi – kwa kiwango kikubwa- inapata fedha kutoka kwa mapato yake[1] takriban Shilingi bilioni 15.1. Ili kujaza pengo lilopo kati ya mapato ya Kaunti na uhitaji uliopo wa Kaunti kutimiza mahitaji yake kulingana na sehemu ya nne ya katiba, Serikali Kuu itahawilisha bilioni 9.5 na milioni 743.1 mtawalia kama mgao sawia wa serikali na kama msaada wa kutegemea.

Kulingana na rasilimali zilizotajwa hapa juu, bajeti ya Kaunti ya Jiji la Nairobi ina zaidi ya shilingi milioni 119.1 ambazo ni za ziada.

Walakini, mwaka uliopita, Kaunti ya Jiji la Nairobi iliweza kukusanya shilingi bilioni 6.8.[2]


<?> Mapato ya Kaunti yatatokana na; kima kinachotozwa na Kaunti, vyeti vya kufanyia biashara za aina moja, vyeti vya ujenzi, malipo ya kuegesha magari na mapato kutokana na rasilimali zingine

2 Ripoti ya mashirika yanayofaidi umma ya mwaka wa 2012/2013

Kufikia hadi asilimia 115 ya mapato haitawezekana kwa kuwa mbinu za kupata mapato zilizopo zimekuwa ngumu ikizingatiwa kuwa mabaraza za miji na vijiji yalitolewa. Bajeti ya Kaunti hazikupata fedha za ufadhili wala zile zitokazo kwa hazina ya mabaraza ya miji na vijiji (LATF) za mwaka wa fedha wa 2013/2014.

### iii. Fedha hizi zitaelekezwa wapi?

Kaunti ya Jiji la Nairobi ina muundo unaozingatia sekta nne za utoaji wa huduma. Hii imeonyeshawa katika **picha ya 4** iliyopo hapa chini.





Picha ya 4: **Muundo Na Mgao kwa Sekta wa Kaunti ya Jiji la Nairobi Mwaka wa 2013/14**

### a. Matumizi ya Kawaida/Malipo ya Mishahara


**Picha ya 4** iliyopo hapa juu inaonyesha kuwa kati ya jumla ya **bilioni 14.9** ya

fedha za matumizi ya kawaida/malipo ya mishahara, **bilioni 10.4** au **asilimia 69.9** zilielekezwa kwa kuwalipa/kuwafidia wafanyakazi katika Bunge na Kamati Tekelezi wa Kaunti. Inatarajiwa kuwa Operesheni na Matengenezo vitachukua **asilimia 18 (bilioni 4.5**). Malipo ya madeni yatachukua takribani **asilimia 11** ya bajeti ya malipo ya kawaida.




Picha Ya 5: **Malipo ya Kawaida/Mishahara ya mwaka wa fedha wa 2013/14 katika Kaunti ya Jiji la Nairobi**

## b. Matumizi ya Maendeleo




Picha ya 6: **Matumizi ya Maendeleo ya Mwaka wa 2013/14**

**Picha ya 6** iliyopo hapa juu ina ashiria matumizi ya maendeleo ya Mwaka wa fedha wa 2013/14 katika Kaunti ya Jiji la Nairobi

**Kwa nini matumizi ya fedha katika Kaunti huwa kinyume na bajeti?**

- Mifumo mibaya ya usimamizi wa fedha
- Ufisadi
- Kuelekeza fedha kwingine, tofauti na ilivyopangwa
- Matumizi ya hifadhi ya fedha yasiyotarajiwa
- Ukosefu wa fedha

- Ufadhili wa fedha mbali na bajeti
- Uangalizi ulio hafifu bajeti inapotekelezwa

## Fomu/Mpangilio wa Kutoa Maombi

198. Malalamishi lazima yawe katika fomu iliyowekwa katika ratiba ya tatu na lazima;

a. Iwe imeandikwa, au imechapishwa;

b. Iwe katika lugha ya Kiswahili au Kingereza na iandikwe kwa heshima na lugha nadhifu;

c. Isiwe imebadilishwa badilishwa katika maandishi na ielekezwe kwa Bunge la Kaunti;

d. Iwe na kichwa katika kila ukurasa - ikiwa ina zaidi ya ukurasa mmoja;

e. Onyesha ikiwa kuna majaribio yoyote ambayo yamefanywa hapo awali ili jambo hilo lishugulikiwe na wanaohusika. Onyesha ikiwa wanaohusika walitoa majibu yoyote;

f. Onyesha ikiwa jibu lilotolewa lilikuwa la kuridhisha;

g. Onyesha ikiwa jambo lililo katika ombi lipo mbele ya mahakama ya kisheria au afisi/afisa wa kikatiba au kisheria;

h. Malizia kwa ombi lililo wazi, kamilifu na la heshima ukikariri uhakika wa nia ya msukumo wa anayefanya ombi/wanaofanya ombi kuhusu swala husika;

i. Kulingana na aya ya (m), ombi liwe na majina, anwani, nambari za

vitambulisho, sahihi au alama ya kidole ya wote wanaotoa ombi – ikiwa ni zaidi ya mtu mmoja;

j. Liwe na sahihi au alama za vidole pekee, itakavyokuwa, na anwani na nambari za vitambulisho kuandikwa moja kwa moja kwa ombi bila ya kuwekwa au kuhamishwa uko;

k. Lisiwe na barua, hati au stakabadhi zozote zilizoongezewa kwalo;

l. Ikiwa ni ombi lililotolewa na mwakilishi kwa niaba ya anayeomba, pia liwe limetiwa sahihi na mwakilishi anayelitoa; na

m. Ikiwa anayetoa ombi hana uwezo wa kutia sahihi, litiwe sahihi na shahidi ambaye atakuwepo wakati anayetoa ombi atakuwa akitia alama katika ombi hilo.

## RATIBA YA TATU

**FOMU YA JUMLA YA OMBI LA UMMA [Taratibu za bunge … (….98)]**

**Mimi/Sisi, Waliotia sahihi hapa chini,**

(Hapa, kwa lugha ya jumla, taja anayetoa/wanaotoa ombi ni akina nani, kwa mfano, wananchi wa Kenya, walio na makaazi mkoa au eneo fulani, wanayakazi mahali fulani, nakadhalika)

**VUTIA umakini wa Bunge la Kaunti kwa yafuatayo**

(Hapa, taja kwa ufupi sasabu zilizokuelekeza kutoa ombi ili lishugulikiwe na bunge la kaunti. Onyesha malalamiko au shida kwa ufupi ukiangazia yaliyo ya kweli/halisi ambayo mwombaji/waombaji wangetarajia bunge la kaunti lizingatie)

**KWAMBA**

(Hapa, thibitisha kuwa bidii imefanywa ili jambo hilo litatuliwe na afisi/afisa husika na kuwa afisi/afisa huyo ameshindwa kutoa jawabu linaloridhisha)

**KWAMBA**

(Hapa, thibitisha kuwa swala linalowasilishwa na mwaombaji/waombaji halipo mbele ya mahakama ya kisheria, au katika afisi/afisa wa kikatiba au sheria yoyote)

**NDIO MAANA kwa unyenyekevu mwombaji/waombaji wanaliomba bunge la kaunti-**

(Hapa, taja ombi kwa ufupi ukisema hatua ambazo mwombaji anatarajia bunge la kaunti litachukua au litaepukana nazo.)

| Jina la mwombaji | Anwani Kamili | Nambari ya Kitambulisho au pasipoti | Sahihi/Alama ya Kidole |
|---|---|---|---|
| ........................... | ......................... | ......................................... | ............................ |
| .......................... | ......................... | ........................................ | ............................ |
| .......................... | ......................... | ......................................... | ........................... |

(Hapa, rudia kwa ufupi yaliyopo katika ukurasa wa kwanza)

| Jina la Mwombaji | Sahihi/Alama ya Kidole |
|---|---|
| ................................................ | ................................................ |
| ................................................ | ................................................ |

(Kurasa Zinazofuata)

Fomu hii inaweza kuwa tofauti kutokana na mazingira ya kila kesi itakavyohitajika.

KITUO CHA SHERIA
LEGAL ADVICE CENTRE
*we care for justice*


## Head Office

**Ole Odume Rd, Off Argwings Kodhek Rd,**
P.O. Box 7483 - 00300, Nairobi, Kenya.
Tel: 254-020-3874220, 387419, 3876290,
Mobile: 0734874221, 0727773991, Fax: 254-020-3876295
E-mail: info@kituochasheria.or.ke

## Branch Office

**Jogoo Rd, Nairobi, Forced Migration Program (FMP), Jogoo Road Plaza**, Jogoo Road,Tel: 202451631, 0736867241, 0720806531

## Regional Office

**Mombasa, Opp Ganjoni Primary School,**
P. O. Box 89065, Mombasa, Kenya. Tel. : 254-041-2230282, 0731129739, 0700638379, Fax: 254-041-2230283
E-mail: msa@kituochasheria.or.ke


*We Care for Justice*